

SAYANSI YA AKILI

Wataalamu wa Sayansi ya Akili Walioidhinishwa



Kupitia Vituo vya Maisha ya Kiroho za Sayansi ya Akili, wataalamu wa kiroho walioidhinishwa husaidia watu kutumia sala ya kuthibitisha kuleta mabadiliko katika maisha yao. Sala haya, yanayojulikana kama "matibabu ya akili ya kiroho," ni maombi ya kuthibitisha ambayo huleta uelewa na mafunzo ya mtaalamu kusaidia wale wanaopenda kubadilisha hali katika maisha yao.

Wataalamu walioidhinishwa wanaweza kukusaidia kuimarisha Ukweli katika fahamu zako binatsi, iwe unakabilia na changamoto au unasherehekea mafanikio. Wanawaunga mkono wengine katika kuunda maisha yenye afya, nguvu, na kuridhisha. Wanajitahidi kuponya nafsi zao na wengine kupitia utambuzi wa nguvu ya ubunifu iliyo ndani yetu sote na kwa kutumia sala chanya ya uthibitisho. Wataalamu hupewa leseni na **Centers for Spiritual Living**. Wanafuata kanuni za maadili kuheshimu faragha yako. Kazi yao imejikita mafunzo ya mabadiliko ya mwanzilishi wa **Science of Mind**, Ernest Holmes. Kanuni inayowaongoza ni kwamba Mungu ndiye kila kitu kilichopo, na kwamba Ulimwengu hufanya kazi kwa mfumo wa sheria za kiroho zinazotabirika.

MATIBABU YA AKILI YA KIROHO

Matibabu ya akili ya kiroho yanategemea imani kwamba tumezungukwa na Akili ya Ulimwengu inayofanya kazi kupitia sheria za asili. Sheria hizi hujibu mawazo yetu, na matumizi ya matibabu ya akili ya kiroho hubadilisha imani zako kuhusu wewe mwenyewe, na hivyo kusababisha mabadiliko katika maisha yako. Kila mmoja wetu yuko huru kuchagua kile cha kuamini, na kwa hivyo tunaweza kutumia Sheria ya Akili kufikiria mawazo ya kujenga au ya kuharibu. Tukitumia Sheria kwa njia ya kujenga, tunaweza kuvutia afya, amani, wingi, maelewano na furaha. Kadri imani yetu katika uwezo wa kutumia Sheria ya Akili inavyokua, uwezo wetu wa kuleta mema katika maisha yetu huongezeka, na kuunda kujiamini na furaha.

JINSI MTAALAMU ANAVYOKUONGOZA

Wakati mwingine tunakuwa karibu sana na hali zetu wenyewe, jambo ambalo hutufanya tushindwe kuona mambo kwa uwazi. Au pengine tunakosa uzoefu unaohitajika ili kuona njia mbadala zinazowezekeka. Mtaalamu aliyeidhinishwa anaweza kutusaidia kuona ukweli wa kiroho unaotuzunguka. Mtaalamu anaweza kueleza jinsi ya kuwezesha uponyaji au kurekebisha hali fulani. Wataalamu wamefunzwa kwa kiwango cha juu katika matumizi ya matibabu ya akili ya kiroho. Watakufanyia sala hii ya uthibitisho na kukuonyesha jinsi ya kuitumia wewe mwenyewe ili mabadiliko unayotamani yawe endelevu katika maisha yako.

KUTUMIA HUDUMA ZA MTAALAMU

Wataalamu wengi hukutana na wateja ana kwa ana au kwa simu. Hatua ya kwanza ni kuelewa tatizo lako na sababu zake. Kisha, mtaalamu atakupa zana za kiroho zilizothibitishwa zinazokuwezesha kupanga mwelekeo wa maisha yako. Mtaalamu wako hufanya kazi kwa usiri, akikusaidia kutambua mema yako. Wataalamu ni wataalamu walioboea, na kikao cha mtaalamu ni kama kikao kingine cha huduma ya kitaalamu. Utaweka miadi na kukutana katika mazingira ya kitaalamu. Wataalamu hulipwa kwa muda wao na utalamu wao katika matumizi ya sheria za kiroho. Ada za huduma hutofautiana, kwa hivyo tafadhali jadiliana na mtaalamu wako kuhusu muundo wa ada.

Unaweza kupata mtaalamu au kituo cha kiroho cha Center for Spiritual Living kilicho karibu nawe kwa kutembelea tovuti ya Centers for Spiritual Living: www.CSL.org.

